ISLAMU WAOMBOLEZA KIFO CHA SHEIKH FARSY

Marehemu Sheikh Abdalla Swaleh Al Farsy.

SISI sote ni wa Mungu, na kwa Mungu tutarudi. Njia aliyopita almarhum ni njia ya haki ya kila mmoja wetu ingawa kila mmoja yuko na siku yake. Kwa wingu hili la msiba lililotukubika ghafula, hatuna budi kurudi kwa Mungu na tukawa wenye subira kwani huno si msiba wa mtu mmoja bali ni msiba wa Waislamu wa Afrika Mashariki yote.

Al allama Sheikh Abdalla Saleh alikuwa ni mwanazuoni uchamungu na uadilifu. Elimu yake bahri aliyokuwa nayo, hata siku moja haikuwahi kumfurisha, kichwa na akaanza kujinata, kujigamba na kujifanya kwamba yeye ndiye bwana wa mabwana. Kuanzia kivazi chake hadi mlahaka wake na watu si mambo ambayo yalimkimbiza kwenye watu bali yalimkurubisha zaidi kwenye mapenzi ya watu.

Ajabu kubwa ni kwamba saa yo yote unapokutana na almarhum hujioni mnyonge hata kidogo mbele yake kwa ile namna atakayoamkuana na wewe na kuongoea na wewe kana kwamba wewe pia umwanachuoni. Sifa hii ndiyo iliyokuribisha watu kwenye watu kwenye darsa za almarhum.

Kuna watu walikuwa wakisikia sifa tu za Sheikh Abdalla, yaani walikuwa hawamjui na hawajahudhuria kwenye darsa zake. Baada ya watu hao kukutana naye mara moja tu walimpenda na wakahudhuria darsa zake mpaka alipoondoka Kenya.

Almarhum alisoma katika kisiwa cha Unguja. Kwa akili yake iliyokuwa kali sana na bidii yake isiyokuwa na mfano, aliweza kujipendekeza kwa walimu wake wote na wakamtambua kama mwanafunzi ambaye amejipwekesha katika nyanja za elimu. Elimu yake haikukita kwenye fani moja lakini ilienea katika fani zote kama vile Fikhi, lugha, Tawhidi, tafsiri na Taareikh pamoja na Hadith.

Almarhum katika siku zake za mwisho hapa Kenya alikuwa na umri wa myaka sabini na mbili, hata hivyo alikuwa akiendesha darasa kwa hamasa na sauti ya mvulana wa myaka ishirini. Hivi ni kusema hakupungukiwa na sauti wala nuru yake ya macho.

SAFINA

Na ingawa Almarhum alikuwa na elimu kubwa kiasi hicho ni ajabu vile alivyokuwa akijua kupanga na kuandaa darsa zake. Hapa nakusudia kusema kwamba hata mtoto ndogo alikuwa akifahamu mafundisho ya Shekhe na pia juu ya ujuzi wake mkubwa huo lakini alikuwa akiweza kufundisha watu vitabu vidogo sana kama vile Safina na pia wasikilizaji watapenda kusikiliza na watafahamu (hadi tuelewe kwamba wanazuoni wengine darsa zao hazifahamiki na mtu wa kawaida kwani hutaka kujionyesha mbele za wasikilizaji kwamba wao ni bahri kubwa).

Kuja kwake Almarhum hapa Mombasa kutoka Unguja ilikuwa ni kama ajali kwani alipotoka huko visiwani, alinuilia kuja kumtazama rafiki yake mpendwa Almarhum Sheikh Muhammed Kassim Al Mazrui ambaye siku hizo alikuwa ameshikwa na ugonjwa wa macho. Wasemavyo watu 'riziki ya mtu haili mtu' ndipo Almarhum akajikuta katika vurugu la uchaguzi wa Kadhi Mkuu wa Kenya, kazi ambayo hakuilalia wala hakuiamkia.

KADHI MKUU

Mwenyezi Mungu alikuwa ameshaliandika, kwa hivyo likawa. Lakini Shekhe alipotawala kama Kadhi Mkuu, haikuwa hamu yake kubaki afisini peke yake. lakini hamu yake kubwa ilikuwa ni kuendesha darsa ili apate kuieneza elimu kwa Waislamu ambao walikuwa na kiu kubwa ya dini yao.

Almarhum alianza darsa zake katika msikiti wa Mabulushi. Baada ya kuondoka katika msikiti huo, alistawisha darsa zake katika Msikiti wa Shibu. Darsa za msikiti huu zilifana sana hasa katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Waislamu walitoka pembe zote na viunga vya Mombasa kuhudhuria darsa, hizo. Msikiti wa Shibu uko Njia kubwa na kwenye kituo cha magari kwa hivyo ilikuwa ni rahisi zaidi watu kuja na kuondoka darasani bila ya kuchelewa kurudi makwao. Darasa hizo za Sheikh ikawa sasa zaendelea kwa kufatana na maombi na mapendeleo ya maratibu wa msikiti.

Hivyo ikawa msikiti mmoja baada ya mwengine inapeleka maombi afisini kwa shekhe ili na wao wafanyiwe darasa. Basi msikiti iliyofata, ni kama hivi: Sakina, Mussa, Kaloleni, Lango la Papa, Marembo, Azhar, Ridhwan, Rahma na wa mwisho ulikuwa Noor.

Lakini darsa za shekhe hazikumalizikia hapo kwani alianza misafara ya Changamwe Likoni Nchi yote ya Digo kufikia Msambweni, Takaungu, Kilifi na Malindi. Halikadhalika alikuwa akisafiri hadi mikoa mengine kama vile Nyanza na Mkoa wa Magharibi kwa shughuli mbali mbali za kidini. Hivi ni kusema kwamba Shekhe hakufa ila ameshafika kila kipembe cha Kenya kuonana na waislamu na kuwatengezea mambo yao. Mwangaza wa elimu yake uliwatoa wengi kizani.

Almarhum hakumalizikia uanachuoni peke yake bali alitia fora katika sifa ya ukarimu. Ingawa shekhe alianza kazi toka mwaka 1936 huko Unguja (alikuwa mwalimu wa skuli, akawa mwalimu wa walimu, na baadaye akawa mwalimu mkuu) lakini mpaka alipokufa, hakuacha milki yoyote ya nyumba, au shamba. Pato lake lote alilitumia kwa kulisha watu wake, kusaidia jamaa zake na kusaidia masikini wa Mungu. Ndio leo twathubutu kusema kwa sauti kubwa kwamba katika Bara la Afrika hajawahi kutokea mawanachuoni ambaye amekusanya sifa zote, kusoma sana, ucha Mungu na ukarimu wa hali ya juu kama shekhe Abdalla.

VITABU

Na bila ya shaka hivi sasa huko aliko mbele ya haki anavuna matunda ya kile alichokipanda huku ulimwenguni. Twaomba iwe ni mavuno ya kheri ya kustarehesha

Angelikuwa hakufanya kazi Almarhum ama kazi yake haikukamilika laiti ingalikuwa aliwacha nyuma yake elimu iliyomo katika vichwa vya watu peke yake, kwani hiyo isingefaidisha vizazi vya mbeleni. Lakini kwa vile ameandika vitabu vingi vya Kiswahili na akaitafsiri Quran Tukufu kwa Kiswahili na akaacha nyuma yake wanafunzi waliobobea elimu na ambao hawachi kuisema haki popote walipo, Wallahi twashuhudia kuwa Shekhe Abdalla amekamilisha kazi yake kama mwanazuoni.

Wanafunzi wake wamesambaa toka Unguja, Pemba, Tanzania Bara, Mombasa hadi Malindi. Jee wote hawa watashindwa kuiendeleza kazi iliyoanzwa na shekhe wao?

Sina budi kama mwislamu kuhubiri mapenzi baina ya waislamu. Yataka tusipendelee kurudia makosa yetu mumo kwa mumo. Mwenyezi Mungu wetu ni mmoja, Mtume wetu ni mmoja, Kitabu chetu ni kimoja na Dini yetu ni moja. Jee ndugu zangu waislamu kuna haja sisi kubugudhiana kila siku na tukazipa dini nyendine fawaida kwamba sisi waislamu hatupendani? Kwa nini hatushikani kwa faida ya vizazi vyetu.

Iwapo sisi watu wazima tumeshakomaa katika utesi jee wata mwataka tabia hiyo pia irithiwe na dhuria zetu? Ndugu zangu waislamu hiyo "Ruhamau Bayna hum" itapatikana lini? Kwani hamjui kwamba sifa hiyo tumesifiwa nayo sisi "Walladhiyna maahum".

Kwa makala yangu haya ya Tanzia natoa mwito kwa aniaba ya waislamu wote wa Mwambao kwa wanazuoni wetu wakae chini na wasuluhishe tafauti zao mara moja kwa faida ya waislamu wa nchi hii pamoja na vizazi vyao. Tumechoka kutafunana sisi kwa sisi wala hatuoni faida tuipatayo isipokuwa twajifanya vichekesho kwa dini nyengine. Natukome ndugu zangu.

ASSALAMA

Na turudi kwenye Quran itwambiayo "Waatasimuu bihabli llahi jamiia walaa tatafarrakuu". Assalama alaykum warahmatullaji wabarakaatuhu.

Rambi Rambi

"Inna lillahi wa inaa ilaybi Rajiuna". Tumepokea habari za kifo cha mwana chuoni wetu mashuhuri Sheikh Abdalla Swaleh Al-Farsy kwa mshutuko mkubwa sana nakimetusababishia huzuni nyingi zisizoweza kuelezeka.

Kamati walimu na wanafunzi wa Hudaa Muslim School ya Guraya Mombasa wanatuma risala ya rambirainni na mkono wataazia kwa jamaa na Ndugu za marehemu kwa msiba huu ulio wafika.

Kazi za Shekhe za alizoacha zitabaki athari yake milele, tafsiri aliyo ifasiri ya Quran kwa lugha ya Kiswahili ndio inayofundishwa ndani ya Madrasa hii na pia kile Kitabu chake cha Maisha ya Nabii Mohammed.

Mungu amuweke pema penye wema.

Omar Islam Faraj MOMBASA.

Kwa niaba yangu na ya Kilabu ya Libati Heroes, napenda kutoa rambi rambi zangu kwa jamaa ya marehemu Sheikh Abdalla Swaleh Al-Farsy aliyefarik, dunia Muscat, Oman. Kifo chake kimetufikia kwa mshituko makubwa na huzuni tele. Ni msiba mkubwa kwa Waislamu wote nchini Kenya. Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi.

ABEID K. SALIM.
MOMBASA

Marehemu Sheikh Abdalla Swaleh Al Farsy katika karamu yake ya kumuaga alipostaafu kama Kadhi Mkuu wa Kenya iliyofanywa katika ukumbi wa Waislamu.

Pichani anaonekana Mkuu wa Mkoa Bw. Galgalo Meya Diwani Rajab Sumba na Mbunge Said Hemed.

PICHA: ABEID KARAMA

Mola amweke Peponi Sheikh Farsy

TULISIKITISHWA sana kwa kifo cha ghafla cha Sheikh wetu, kipenzi chetu, Allama Sheikh Abdalla Swaleh Al-Farsy kilichotokea jumatano tareikh November 8, 1982 usiku. Hakika ni msiba mkubwa sana kwetu kwa kuondokewa na mtu mkubwa kama huyu. Mwenyezimungu amueke mahali pema peponi na hao watu wema walipigania haki, Amin.

Almarhum Sheikh Abdalla alikuwa kila wakati akiusia watu washikamane na mwendo wa Mtume SAW. Akikabiliana na kila matusi ya wale wanaozuia haki isienezwa pasi na kujali. Akimpenda kila mtu awe mzuri au mbaya na alikua akilipa jema kwa ovu na akisema na kufanya mazuri. Alhamdulillahi wengi tumeiona haki na tumeifuata. Tumeyajua ya Mungu na Mtume wake ni yapi na ya kuzuliwa na watu ni yapi.

Ingawa yeye ameondoka lakini mafundisho yake yatasalia milele na milele Inshallah. Tafsiri yake ya Qurani pamoja na vitabu mbali mbali alivyotunga vitasomwa na kufuatwa hata ni vizazi vitakavyokuja. Inshallah ya Bid a yataondoka na ya Sunna yatasalia, Amin.

Mwenyezimungu amueke peponi, awape moyo wa subra watu wake na awaletee kila kheri badili yake, Amin.

Ali Salim Muhsin na wenzake. MOMBASA.

JISHINDIE

MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD NO 151

KWENDA KULIA:

2. Samaki wa maji ya baridi (ziwa)
8. Ufupi wa ana mkuki
9. Tapia, kimbilia
10. Tapanya, weka mbalimbali
11. Mti wa mahindi au mtama
13. Baa
14. Asali
17. Pamoja na
18. Jina la Kijaluo
21. Nikahi arusi
22. Unywele uliyo juu ya jicho
23. Aitoe maganda

KWENDA CHINI:

1. Uzi mnene
2. Ghairi
3. Afunga ndoa
4. Jina la Kiume
5. Kinyume cha hana
6. Uliyoruzukiwa, chakula
7. Jina la zamani la shirika la ndege Afrika Mashariki
12. Ujuzi uhodari
14. Upeleke ujumbe wa kuoa
15. Ikimbilie, itapie
16. Neno la kuitikia
18. Angalia, tizama
19. Wingi wa yake ukizipanga herufi sawa
20. Sehemu ya kiwiliwili.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 150

1. Kibwana Juma Mzee Sanduku la Posta 85404 Msa.
2. Athman Abdallah Ali Sanduku La Posta 29 Kilifi.
3. H. J. Chika Sanduku La Posta 90520 Mombasa

Washindo waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK.*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 150 —

KWENDA KULIA:

1. MAGUGU, 5. PUMU, 7. SONARA, 8. BT, 9. A.A., 10. MBOGO, 12. ANGIKA, 14. TU, 15. AU, 16. UMUKA, 18. UMO, 19. LAU.

KWENDA CHINI:

1. MASHUA, 2. UTAMBI, 3. UPANGA, 4. OMBA, 6. UTAMU, 10. MGUU, 11. OKOA, 13. NAMI, 14 TIMU, 17. KU.



JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

Shindaano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-Shirt maridadi. Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa.
Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri *COASTWEEK* Sanduku La Posta 87270 Mombasa, Kenya.
Siku ya Jumatano tarehe November 24, 1982 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.